

1013/2

**KISWAHILI, KARATASI YA PILI
MWIGO
MARCH 2019
MUDA : SAA TATU**

MAAGIZO

- a) Andika jina na nambari yako kwenye nafasi ulizoachiwa.
- b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
- c) Mtihani huu una sehemu mbili kuu: sehemu ya A, **FASIHI** na sehemu ya B, **MBINU ZA KUFUNDISHIA**.
- d) Jibu maswali **MATATU** katika sehemu ya A. swali la kwanza ni la **LAZIMA**. Chagua maswali mengine mawili kutoka kwa swali la 2, 3, au 4. (Swali la tamthilia, riwaya au Hadithi fupi).
- e) Usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja.
- f) Jibu maswali **YOTE** katika sehemu ya B.
- g) Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu
- j) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

SEHEMU	SWALI	UPEO	TUZO
1	1	15	
	2a	15	
	2b	15	
	3a	15	
	3b	15	
	4a	15	
	4b	15	
2	5	35	
	6	20	
JUMLA			

USHAIRI**SAUTI YA DHIKI – ABDALLATIF ABDALLA**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia. (alama 15)

1	Mkono inuka Upate ya'ndika Ipate someka Wapate yashika	inuka hima kwa khati njema wenye kusoma na kuyapima	twaa kalamu hino nudhumu waifahamu yaliyo humu
---	---	--	---

2	Kuandika anza Na mimi naanza Alivyonifanza Wapate jitunza	anza 'sikawe kisa chenyewe nao wajuwe salama wawe	mkono wangu cha mlimwengu waja wenzangu hawa ndu zangu
3	Mja kikudhani Nikamuamini Kumbe mwafulani N'shabaini	sikudhaniya hafikiria hakuzoweya ingawa baya	tanizunguka hatageuka kuaminika lishanifika
4	Menitenda kisa 'mezinduka sasa Ni yangu makosa Sikuwa napasa	kisa adhimu n'shafahamu najilaumu hata sehemu	mja mcheni najuwa kwani kumuamini kumthamini
5	'Meniua mja Mjaye daraja Muonapo mja Asije akaja	mja ni nduli nda katili kaani mbali (kwani habali)	tahadharini hana Imani mjitengeni kuhasirini
6	Mja hana haya Mja ni mbaya Na ukisha ngiya Mmoja kwa miya	baya hazimo hatimba shimo azome zomo ndiye hayumo	kwake usoni ungiye ndani furaha gani baya kundini

Maswali

- i) Taja bahari tatu zinazijitokeza katika shairi hili na utoe sababu. (alama 3)
- ii) Taja maudhui ya shairi hili (alama 2)
- iii) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- iv) Uhuru wa mshairi umetumikaje katika shairi? (alama 2)
- v) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

2. UPEPO WA MVUA - Jeff Mandila

Jibu swalil a au la b

- a)i "... poeni moto... hadi sasa sijajua mnalilia nini."
- i) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- ii) Fafanua sababu za kilio kinachorejelewa. (alama 11)

AU

- b) Dau la mnyonge haliendi joshi. Eleza ukweli wa methali hii kwa kurejelea uhusika wa Kidani. (alama 15)

3. HADITHI FUPI

VAZI LA MHUDUMU na hadithi nyingine

Jibu swalil a au la b.

- a) “... jizee lenye sura mbaya ajabu, macho makubwa kama vikombe na pua zilizotanauka kama za sokwe mtu...”
 i) Eleza muktadha wa maneno haya ukirejelea hadithi WALIMUUZA DADANGU
 (alama 4)
 ii) Fafanua sifa tatu msemaji ni? (alama 6)
 iii) Jadili maudhui ya utamdu kama yalivyodokezwa katika hadithi. (alama 5)

AU

- b) Thibitisha kuwa 'Mnyonge hana haki' ukirejelea hadithi ya “*Maisha Uso Mkesha*”. (alama 15)

4. RIWAYA :PENDO LA KARAHA – John Habwe

Jibu swalil a au b

- a) Kwa kurejelea wahusika watano eleza ufaafu wa anwani PENDO LA KARAHA.
 (alama 15)

AU

- b)ii “ Mama, mwanao hakujisajili hapa katika data yetu. Labda alikuwa na mpango na wakala wa kibinafsi ambaye hakuufahamisha ubalozi huu. Sasa itabidi umtafute wakala huyo.”

- i) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
 ii) Eleza sifa za wakala wa kibinafsi anayezungumziwa katika dondo hili. (alama 6)
 iii) Kwa kutumia mifano mwafaka eleza mbinu tano za lugha zilizotumika katika riwawa hii. (alama 5)

SEHEMU YA PILI: MBINU ZA KUFUNZIA

5. Jibu maswali yote kutoka sehemu hii.

Unanuia kufunza kipindi cha matumizi ya kamusi kwa wanafunzi wako wa darasa la tano kwa kutumia mifano halisi fafanua mambo **kumi** unayoweza kufunza katika kipindi hiki. (Alama 20)

- a) Eleza faida tano za mwalimu kutayarisha na kuhifadhi vitendea kazi vifuatavyo.
(alama 15)

Rekodi za kazi

i)Kumbukumbu za tathmini

ii)Maandalizi ya vipindi

6 Eleza hatua utakazofuata kufunza sentensi katika darasa la tatu. (alama 20)